# Maagizo ya Kichunguzi cha Uandishi kwa Wanafunzi walio na Elimu Rasmi Iliyotatizwa/Isio thabiti (SIFE)

## Maagizo ya Kichunguzi cha Uandishi

Madhumuni ya Kichunguzi hiki cha Uandishi cha lugha ya nyumbani au msingi ni kupata wazo la jumla la stadi za kuandika za Wanafunzi watarajiwa ambao Elimu Rasmi Imetatizwa/Si thabiti (Students with Interrupted/Inconsistent Formal Education, SIFE). Kichunguzi kinaweza kutumiwa kwa mtu binafsi au kwa kikundi na wanafunzi wanapaswa kupewa dakika zisizozidi 15 ili wakamilishe kazi. Matokeo ya kichunguzi hiki yanapaswa kutumiwa pamoja na tathmini nyingine ili kukadiria uwezo wa kuandika wa wanafunzi watarajiwa wa SIFE, ambay inaweza kuchangia kwa uamuzi wa mafunzo sahihi ya uandishi.

## Maagizo ya Usimamizi:

Kabla ya kuanza kutumia Kichunguzi, tambua lugha ya nyumbani au ya msingi kama ilivyotambuliwa kutoka kwenye Hojaji ya Lugha ya Nyumbani (Home Language Questionnaire, HLQ). Kwa sasa, Kichunguzi kitolewa katika lugha zifuatazo:

- Kiarabu
- Kibangla
- Kibama
- Kichina
- Kifaransa
- Kifulani
- Kikrioli cha Haiti
- MaayMaay
- Kinepali
- Kirusi
- S’gawKaren
- Kisomali
- Kihispania
- Kiswahili
- Kiurdu

1. Ikiwa mwanafunzi ataandika kwa lugha ambayo haijaoorodheshwa hapo juu, anaweza kuandika kwa lugha hiyo akitumia kidokezo na mafunzo ya Kiingereza ambayo yametafsiriwa katika lugha yake ya nyumbani au ya msingi. Fahamu kuwa toleo la Kiingereza la Kichunguzi linapaswa kutumiwa kama chanzo cha tafsiri pekee na halipaswi kutumiwa kwa wanafunzi wa Kiingereza.
2. Mkufunzi anaweza kujaza katika sehemu ya maelezo msingi ya mwanafunzi (jina, tarehe ya kuwasili, tarehe ya kusajiliwa n.k.). Mafunzo yoyote ya kunena yanapaswa kutolewa katika lugha ya nyumbani au ya msingi ya mwanafunzi.
3. Wambie wanafunzi kuwa wataandika katika lugha yao ya nyumbani au ya msingi. Waambie kuwa hili si jaribio, lakini wahimize wajitahidi wawezavyo.
4. Unaweza kujibu maswali ya msingi kuhusu kazi, lakini uepuke kufafanua, kupendekeza mawazo, au vinginevyo kumsaidia mwanafunzi moja kwa moja. Wanafunzi hawapaswi kutumia kamusi wakati wa kazi hii.
5. Wanafunzi wanapaswa kuhimizwa kuandika kadri wanavyoweza na kupewa karatasi ya ziada ikiwezekana.
6. Uandishi wa mwanafunzi unapaswa kuwekewa alama na mnenaji halisi wa lugha ya mwanafunzi.
7. Tafadhali fahamu kuwa matokeo katika Kichunguzi cha Uandishi cha SIFE si kiashiria cha hali ya SIFE.

**Maagizo ya Kuweka Alama:**

Baada ya mwanafunzi kukamilisha shughuli, mtoa alama anapaswa kuamua ngazi ambayo inaelezea vizuri uandishi wa mwanafunzi katika kila kategoria (Maudhui, Mpangilio, Mbinu na Stadi za Lugha, Ubora na Utata wa Lugha). Kiwango cha stadi ambayo mara nyingi huwakilisha uandishi wa mwanafunzi (0 – 3) huamua alama ya jumla ya mwanafunzi kwenye utaratibu.

Kwa mfano, mwanafunzi anayepokea alama ya 3 katika Maudhui, Mpangilio, na Mbinu na Stadi za Lugha na alama ya 2 katika Ubora na Utata wa Lugha atapokea alama jumla ya 3.

Tafadhali fahamu kwamba matokeo ya Kichunguzi cha Kuandika ni sehemu ya data ambayo inapaswa kutumiwa pamoja na hatua nyingine ili kukadiria uwezo wa kuandika wa mwanafunzi mtarajiwa wa SIFE.

| Kufasiri alama ya mwanafunzi kwenye Kichunguzi cha Uandishi | |
|---|---|
| **Mara nyingi 3** | Mwanafunzi anaonyesha ufahamu wa kutosha katika uwezo wake wa kuandika. |
| **Mara nyingi 1 na 2** | Mwanafunzi anaonyesha ufahamu wastani katika uwezo wake wa kuandika. |
| **Mara nyingi 0** | Mwanafunzi anaonyesha ufahamu mdogo katika uwezo wake wa kuandika. |

| Jina: | | Umri: |
|---|---|---|
| Tarehe: | Lugha ya Nyumbani: | |
| Tarehe ya Kuwasili Marekani: | Nchi Aliyozaliwa: | |

Kichwa cha uandishi wako: ________________________________

**Kidokezo**

Kwa zoezi hili, andika kuhusu mchezo unaopenda kucheza. Tumia nafasi ifuatayo kuandika aya moja au mbili kuhusu mchezo unaopenda:

Kumbuka kujumuisha katika uandishi wako:

- ☐ Jina la mchezo unaopenda
- ☐ Jinsi ya kuucheza mchezo
- ☐ Maelezo kuhusu mchezo
- ☐ Kumbukumbu zozote unazoweza kuwa nazo za kucheza mchezo
- ☐ Sababu za kuupenda mchezo huo

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

## Utaratibu wa Kichunguzi cha Uandishi

| | 3 | 2 | 1 | 0 |
|---|---|---|---|---|
| **Maudhui** | Uandishi unaoeleweka na wenye kutoa maelezo muhimu na unamshirikisha msomaji. Yanaonyesha mawazo mazito kuhusu zoezi lenyewe | Suala la mada linaeleweka lakini linakosa maelezo. Yanaonyesha ufahamu kamili wa kazi. | Maelezo kidogo yatolewa, yanaweza kujumuisha maelezo yasiyo muhimu. Yanaonyesha ufahamu mchache wa zoezi lenyewe. | Uandishi umepotoka au una maelezo machache au hauna maelezo muhimu. Yanaonyesha ufahamu mdogo au kutoelewa zoezi lenyewe. |
| **Mpangilio** | Uandishi una mshikamano na unaeleweka, wenye mtiririko mzuri wa mawazo. | Uandishi unaweza kutenganishwa lakini msomaji bado anaweza kuelewa maana iliyokusudiwa. Unaweza kukosa mpangilio kiasi na/au kukuzwa kidogo. | Uandishi hauna mpangilio na haujakuzwa. Ni vigumu kuelewa, na mpangilio wa mawazo unazuia ufahamu. | Uandishi hauleti maana. Sehemu yake inaweza kuwa nakala ya kidokezo. |
| **Mbinu za Stadi za Lugha** | Matumizi ya sarufi yanapanua maelezo na uandishi ni fasaha. Makosa ya tahajia hayazui ufahamu. Uzingatiaji mkubwa wa stadi za uandishi. | Sarufi inaweza kusababisha mkanganyiko kidogo kuhusu maana. Makosa katika stadi za uandishi na tahajia yanaweza kuzuia ufahamu. | Makosa mengi ya sarufi, stadi za lugha na tahajia yanazuia ufahamu. | Sarufi na tahajia isiyo sahihi inafanya uandishi kutofahamika. Hakuna matumizi ya stadi za uandishi yameonyeshwa. |
| **Ubora na Utata wa Lugha** | Msamiati na muundo wa sentensi zinatofautiana na ni sahihi. | Msamiati na muundo wa sentensi ni sahihi. | Msamiati na muundo wa sentensi si sahihi kwa wanafunzi. Makosa ya mara kwa mara yanazuia ufahamu. | Msamiati na muundo wa sentensi haufahamiki wala si sahihi. Huenda kusiwe na jibu kabisa. |